

NGUVU

Utangulizi

Kwas miaka mingi nime tafuta Bwana ili aachilie mazingira mazuri ya uwepo wake, nguvu na utukufu wake kudhihirika. Tumeona na kujua matokeo ya yale Bwana ametufunulia.

Ikiwa unatafuta mwondoko wa Mungu katika maisha yako, jamii au huduma tafadhali zingatia kanuni kumi kuhusu nguvu katika kijitabu hiki- nina hakika kuwa kanuni hizi zitayapanga mazingira mazuri ya Roho Mtakatifu kujidhihirisha na kujifunua mwenyewe katikati yetu. Atakuwa na uhuru wa kufanya kila alitakalo kwa utukufu wa Baba katika jina la Yesu. Nao watu watajua kuwa Bwana amekuwa miongoni mwao.

Ufalme wa mungu, nguvu na utukufu.

Tunasema katika sala ya Bwana, “Kwa kuwa ufalme ni wako, na nguvu na utukufu, hata milele amina” Kwa hivyo, wakati ufalme wa Mungu unaponawiri katika maisha ya mtu, nguvu na utukufu wa Mungu huwa matokeo yake.

Yesu alisema,

a, *”Lakini mimi nikitoa pepo kwa Roho wa Mungu, basi ufalme wa Mungu umekwisha kuwajia”* (Mathayo 12:28)

b, *”Amini, amini, nakwambia, mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi kuuona ufalme wa Mungu”.* (Yohana 3:3)

c, *”Wakati umetimia, na ufalme wa Mungu umekaribia, tubuni, (ondokeni kwa njia zenu na kufahamu kwenu) na kuiamini injili.* (Mariko 1:15)

d, *”Pozeni wagonjwa, fufueni wafu, takaseni wenye ukoma, toeni pepo, mmepata bure toeni bure”* (Mathayo 10:1, 7-8)

e, *”Amini nawaambia, pana watu kati ya hawa wasimamao hapa ambao hawataonja mauti kabisa, hata watapouona ufalme wa mungu umekuja kwa nguvu.* (Mariko 9:1)

f, *”Msisumbuke basi mkisema, tule nini? Au tuvae nini?.....bali utafuteni kwanza ufalme wake na haki yake, na hayo yote mtazidiwa” Basi msisumbuke ya kesho, itajisumbukia yenyewe”* (Mathayo 6:31, 33-34)

g, *’Ufalme wako uje, mapenzi yako yatimizwe, hapa duniani kama huko mbinguni ’* (Mathayo 6:10)

Katika ufalme wa Mungu hakuna tena uchungu, kuteswa, huzuni, magonjwa, kutamauka au mauti (Ufunuo 21:3-5) kwa nini? Ufalme wa Mungu umekuja katika nguvu na utukufu. Neno la Mungu kupitia mtume Paulo linasema, *“Maana ufalme wa Mungu hauwi katiika neno bali katika nguvu”* (1 wakorintho 4:20) *“Neno la Mungu na kuhubiri kwangu hakukuwa kwa maneno ya hekima yenye kushawishi akili za watu, bali kwa dalili za Roho na za nguvu, ili imani yenu isiwe katika hekima ya wanadamu, bali katika nguvu za Mungu”* (1 wakorintho 2:4-5) ufalme wa Mungu huja na nguvu za Mungu na utukufu. (Ufunuo 11:17) sauti kuu kutoka mbinguni ilisema *“Sasa kumekuwa wokovu, na nguvu, na ufalme wa Mungu wetu, na mamlaka ya Kristo wake.* (Ufunuo 12:10)

Watu wanapomwamini Mungu, kupanuka kwa ufalme wake katika maisha yao huleta hekima, nguvu, mamlaka na utawala wa Yesu Kristo. Wanabadilika na kuwa viumbe wapya, wana wa

Mungu.(Yohana 1:12-13) Wakati waaminio katika matendo ya mitume walipojazwa Roho Mtakatifu, wakiongea kwa lugha mpya, nguvu kutoka mbinguni ziliwajia ili wafanye kazi za ufalme wa Mungu sio kuongea tu maneno. (Matendo ya Mitume 1:1-8. 2:1-4) Yesu alianza kulidhibitisha neno lake kupitia wanafunzi wake kwa ishara na maajabu ya nguvu zake.

“Akawaambia, Enendeni ulimenguni mwote, mkaihubiri injili kwa kila kiumbe. Aaminiye na kubatizwa ataokoka, asiyeamini atahukumiwa. Na ishara hizi zitafuatana na hao waamino, kwa jina langu watatoa pepo, watasema kwa lugha mpya, watahika nyoka, hata wakinya kitu cha kufisha hakitawadhuru kabisa, wataweka mikono juu ya wagonjwa nao wagonjwa watapata afya. Basi Bwana Yesu, baada ya kunena nao, akachukuliwa juu mbinguni, akaketi mkono wa kuume wa Mungu. Nao wale (wanafunzi) wakatoka wakahubiri kote kote, Bwana akitenda kazi pamoja nao, na kuthibitisha lile neno kwa ishara zilizofuatana nalo.(Mariko 16:15-20)

Kwa hivyo, Bwana anataka kufanya zaidi kuliko watu kuongea kumuhusu (au upendo wake na matendo yake) tu. Anataka tufanye yale tunayosema kupitia kwake. Anataka kudhihirisha nguvu zake na utukufu ili uwepo wake na ufalme wake ustawishwe katika na miongoni mwa watu wake wanaomwamini nakumtumainia . Sifu Bwana! Na nguvu za Mungu zitayageuza maisha na hali zetu.

Kama mtoto nililelewa katika jumuiya ya kikristo. Nilifundishwa kuwa Biblia ni ukweli wa Mungu na neno takatifu kwa watu wake ambalo limeandikwa na wanadamu lakini wakiongozwa na Roho Mtakatifu. Nilifunzwa kuwa Bwana hupenda kila mtu lakini lazima watu waupokee upendo wake na wazaliwe tena. Mwanadamu ametengwa naMungu naye huhitaji mwokozi. Yesu kristo ni Mungu aliyekuja kwa umbo la mwanadamu kuishi, kufa na kufufuka kutoka wafu ili atuokoe.Yeye aaminiye hivyo na kuziacha njia zake(kutubu)kwa mungu ataokoka sio kwa matendo (kazi yake) lakini kwa imani yao katika Yesu Kristo kama Bwana na mwokozi. Damu ya Yesu ndio dhabihu inayotupatia uhai katika Mungu.

Nilifunzwa kuwa Bwana amenipatia sheria ambazo zimeandikwa katika roho yangu (Wahebrania 8:10) kunionyesha jinsi ya kumpenda pamoja na watu wa ulimwengu wangu ili nijue namna ya kuishi katika ufalme kama mtoto aliyebarikiwa. Nilifunzwa ahadi za Mungu ili zinionyeshe namna ya kukua katika cheo cha utimilifu wa sura ya Kristo.

Kupitia kulisoma neno la Mungu, nilijifunza jinsi Mungu huwapenda na kuwatunza watu wake na mipango mizuri aliyonayo kwa maisha ya kila mtu, ikiwa watautii mwongozo wake na maagizo. Uwepo wa Bwana, baraka na wokovu ni za kweli na hunikaribia. Nilimpenda Yesu zaidi kuliko mimi binafsi au chochote kile katika maisha yangu.

Hata hivyo nilikuwa na maswali ambayo yalinifanya nimtafute Mungu kuyahusu. (Yakobo 1:5-8, Yeremia 33:2-3). Alinifunza jinsi ufalme wa Mungu (uhai) humzunguka Mungu sio binadamu. Wakati binadamu anapoingia katika ufalme wa Mungu kwa kumpokea na kuamini upendo wa Mungu kupitai Yesu Kristo, maisha ya kweli katika mwanadamu huanza.

AMINI MUNGU

Kile Mungu anachotaka kutoka kwetu ni kumwamini, jambo linalodhihirisha upendo wetu kwake.

Tunapomwamini, anapata nafasi ya kufanya yale yote asili yake ya upendo hutaka kufanya. Hakuna lisilowezekana au gumu sana kwa Bwana . Kwa hivyo ninapomwamini na kutii namna anavyoniongoza,nafungua uwepo wake usio kimo na nguvu za upendo wake, hekima,ukarimu, kinga, kutunza na uwezo wake. Hivyo nguvu zake na uwepo wake huchukua nafsi yake ili kuangamiza kazi za mwovu shetani ambaye amekuja kuiba, kuua na kuangamiza. Kuamini na kutii hustawisha ufalme wa Mungu ndani ya anayeamini sasa. Wakati Yesu arudipo, atastawisha ufalme wake kila mahali, milele.

Mwanadamu anakubali upendo wa Mungu na nguvu zake kwa kumpa Bwana sifa, shukrani na utukufu. Kweli Bwana amefanya, anafanya na atafanya mambo makubwa kwa wale wanaoamini na kumpa Bwana sifa, shukrani na utukufu. Kweli bwana amefanya, anafanya na atafanya mambo makubwa kwa wale wanaoamini na kumpa nafasi adhihirishe ukuu wake.

Ili jambo hili kutendeka lazima watu wamtumainie Bwana katika kila hali (Mithali 3:5-6) wakitafuta mwongozo wake na wakifanya kile anachosema. Wakati Mungu alikuwa akinifundisha kuhusu uponyaji(kwa muda wa miaka mitano), aliniambia, “Mwana ikiwa huwezi kufanya, hakuna anayeweza!”. Nililazimika kujua wakati nimeomba, Mungu hufanya lile asemalo angelifanya.

Bwana alinionesha jinsi watu wake wanavyoangamia (Hosea 4:6) na jinsi wanavyodunisha nguvu zake maishani mwao kwa sababu hawajamwamini Bwana badala yake , wamekimbia chemichemi zingine kuliko yeye ili wapate upendo, hekima,kinga,ukarimu,ushauri,uponyaji na hata wokovu. Wengine wanasema Mungu aliwaambia wafanye hivyo wakati Mungu amekataa jambo kama hili.Marafiki msiruhusu kutoamini kuiba imani yenu katika neno la Mungu na njia za Roho wake Mtakatifu. Usimtumainie mwanadamu na njia zake zaidi ya Mungu.

“Kanisa” la mwanadamu linaogopa nguvu za Bwana. “Bwana akaniambia,” Watu wangu wanataka kufanana nami lakini ili kufanana nami hawana budi kutamani sio tu tunda la Roho wangu(tabia) (Wagalatia 5). Lakini pia udhahiri wa Roho wangu. (1 wakorintho 12)

Bwana anatafuta mmoja na kupita kwake na kwake aweza kuzionehsa nguvu zake na utukufu. (11 Mambo ya nyakati 16:9). Alimwambia mfalme Asa kuwa akimtegemea atapata ukombozi. Wakati mfalme Asa wa alipigana vita na mfalme wa shamu na majeshi yake bila kumtegemea Bwana,alishindwa. Baadaye alifariki kutokana na ugonjwa wa miguu kwa sababu hakutafuta msaada wa Bwana bali waganga (Mambo ya nyakati 16:7-12).

Neno linasema,”*Mtu wa kwenu amekuwa hawezi? Mgonjwa na awaite wazee wa kanisa (Wachungaji) nao wamwobee, na kumpaka mafuta kwa jina la Bwana. Na kule kuomba kwa imani kutamwokoa mgonjwa yule na Bwana atamuinua; hata ikiwa amefanya dhambi atasamehewa. Ungameni dhambi zenu nyinyi kwa nyinyi, na kuombeana, mpate kuponywa. Kuomba kwake mwenyewe haki kwafaa sana, akiomba kwa bidii.*

Kuna utata hapa kwa sababu watu wengi katika jumuiya ya kikristo wakiwepo wachungaji huliamini neno hili. Hii ndio sababu watu hawapati matokeo ya Mungu. Tanabahi, ni ombi la imani na haki(kutii) litakalomponya mtu. (Yakabo 5:13-16)

Ikiwa sisi kama watu wa Mungu tutaziona nguvu za Mungu na kupokea matokeo yaliyo yake, hatuna budi kutii neno lake na vile vile mwongozo wa Roho wake Mtakatifu katika kila hali. Ikiwa Mungu aliyeumba ulimwengu kwa kunena neno lake hawezi kufanya hivyo nani aweza-daktari,

mtetezi,majeshi,wewe binafsi?

“Mungu si mtu, aseme uongo; wala si mwanadamu ajute;(abadili mawazo yake) Iwapo amesema, hatalitenda? Iwapo amenena hatalifikiliza?” (Hesabu 23:19)

Kwa miaka neno la Bwana Yesu limeniunguza ndani yangu,”
Kwa wale wanaoamini,matendo niyatendayo watayatenda”

“Amini, amini, nawaambieni, yeye aniaminiye mimi, kwa kazi nizifanyazo mimi yeye naye atazifanya, naam, na kubwa kuliko hizo atafanya, kwa kuwa mimi naenda kwa baba, nyinyi mkiomba lolote kwa jina langu, hilo nitalifanya, ili baba tatukuzwe ndaniya mwana. Mkiomba neno lolote kwa jina langu nitalifanya. Mkinipenda mtazishika amri zangu(Yohana 14:12-15)

Ikiwa huwezi kuamini kuwa Yesu atafanya ayasemayo, basi hutamwona Yesu akizifanya kazi kubwa kupitia kwako.

Yesu alisema,”*Na iwe kwako kulingana na imani yako” wanafunzi wakamuuliza Yesu.”Mbona hatukuweza kumtoa pepo?”(Mathayo 17:19) Yesu akawaambia, “Kwa sababu ya upungufu wa imani yenu. Kwa maana amini nawaambia mkiwa na imani kiasi cha punje ya haradali mtauambia mlima huu, ondoka hapa uende kule, nao utaondoka, wala halitakuwako neno lisilowezekana kwenu. (Mathayo 17:20-21)*

Je, Yesu anasema uongo?Ikiwa sivyo kwa nini hatuoni mambo haya yakitendeka mahali kwingi? Kumbuka, kwa wale waniaminio(Yesu) lolote watakaloliomba kwa jina langu hilo nitalifanya kwa utukufu wa Baba (Yohana 14:12-14) Bwana atalifanya lolote lile kwa utukufu wake. Ni kwa utukufu wa Mungu tunapomwamini na kumtii.

”Basi atukutuzwe yeye awezaye kufanya mambo ya ajabu mno kuliko yote tuyaombayo au tuyawezayo, kwa kadiri ya ya nguvu itendayo kazi ndani yetu; naam atukuzwe katika kanisa” (Waefeso 3:20)

Kile kinachozuia nguvu za Mungu na mapenzi yake kwetu ni mawazo yetu. Bwana anataka kutupenda, kututunza, kutukinga, kutukarimia na kutupigania. Bwana anataka kuokoa, kukomboa,kuwezesha, kupa moyo na kutupa nguvu . Anataka kutuongoza , kutuupatia hekima , ufanisi na kutuongoza katika yote yote mazuri na katika mipango yake mizuri .

Ikiwa tutamwamini, ikiwa tutamruhusu, ikiwa tutamtii, tutaona haya yote yakifanyika. Huko Nazareti Yesu hangefanya yale ambayo Bwana alitaka yafanywe kwa sababu ya watu kutoamini kwa wakaazi wake.

Kwa miaka mingi , kwa jina la Yesu, tumeona mambo sawa na yale Yesu alifanya. Vipofu wanaona, visiwi wanasikia, viwete watembea, bubu waongea, waliovia wanapona waliokadamizwa wafurahi, tasa wapata watoto, waliotamauka wapanga mipango, mawimbi hukoma, amani huwajia waliosumbuka, wafu hufufuka, mioyo iliyovunjika hupona, wenye kiburi huzushwa, waliozushwa huinuliwa, mahusiano huponywa, wale ambao hawajaokoka huokoka,wasiotii hutii, watu waliojazwa Roho wa Mungu hunena kwa lugha mpya.

Maisha yaliyobadilishwa ndiyo ufalme na nguvu za Mungu zinahusu. Kwa kuongezea, ufalme wa

Mungu hauhusu maneno mbali matendo. Katika jina la Yesu ,watu hutubu,wanaokoka,hupona,hukombolewa na kuingizwa kwenye ufalme wa Mungu. Mianza mipya ni matokeo ya kuguzwa na Roho Mtakatifu wa Mungu. Furaha katika na kwa Mungu hufurika katika maisha ya watu yaliyokuwa hayana chochote, akiyajaza kwa matumaini, imani, amani na upendo katika Roho Mtakatifu. Ni furaha iliyoje na baraka kuhusika, kuamini, kusifu na kutii Bwana Yesu akiwaweka watu huru leo! Ndio, “Yesu ni yule yule jana, leo na milele (Waebrania 13:8).

Hakuna kingine chochote kinacholeta utambuzi, furaha, msisimko na kutia ladha, kuliko kuhusika katika huduma ya Roho Mtakatifu, katika jina la Yesu; kuona kicheko cha watu, machozi ya furaha na matarajio ya mabadiliko makubwa zaidi na nafasi zaidi za kesho. *“Basi mwana akiwaweka huru mtakuwa huru kweli kweli”* (Yohana 8:36)

Ndipo, Bwana atafanya kile alichohidi. Je, waamini hivyo? Unatarajia hivyo?.

Nilipokuwa nikisoma Luka 5:17, Bwana alinihudumia kuwa wakati Yesu alipokuwa akifundisha, “Uweza wa Bwana ulikuwapo apate kuponya wangojwa” Alinifunulia kuwa kuna hali ambayo Roho Mtakatifu hutembelea katika nguvu.

MAZINGIRA YA ROHO MTAKATIFU

Kanuni ya nguvu za kwanza.

JUA NA UAMINI KUWA BWANA NI MWENYE UPENDO, HUWEPO,MWENYE HURUMA NA NGUVU.

Bwana anataka na anaweza kuwapenda watu wanaomwamini. Yeye ana mipango mizuri ya kuwafanikisha kiroho, kifikra, kifedha na katika mahusiano yao. Bwana ni Mungu wa imani, tumaini na upendo. Yeye huwapa watu wake sifa hizi ili waweze kuwa na maisha yaliyobarikiwa sasana hata milele pamoja naye. Anataka na anaweza kufanya miujiza kwa watu wake, kulitukuza jina lake na kuwabariki watu wake leo. Yesu alikuja na kupitia maisha yake na kufufuka kutoka kwa wafu, aliangamiza kifo na kazi zote za mwovu shetani. Hakuna lililo gumu kwake Mungu au kwa watu wake katika jina la Yesu.

Kanuni ya nguvu ya pili.

WATU WANA MAHITAJI YA KUTIMIZWA

Mahitaji hayamsukumi Mungu kutenda. Bwana ajua mahitaji yetu yote. Kwa sababu mahitaji yapo hakumaanishi Bwana atakutana nayo. Bwana anataka kukutana nayo lakini anamgonja mtu amwombe na amwamini. Tumepeva kila kitu tayari kupitia Yesu Kristo. Lazima tupokee kwa imani katika Yesu, tukijua kuwa kilichotarajiwa kwa uovu katika dunia, Mungu atakigeuza kuwa chema kwa ajili yetu na utukufu wake . Watu ambao wamebarikiwa ndio wanaoatambua jinsi wanavyomhitaji Mungu katika maisha yao na hali zao. Wao watajazwa (Mathayo 5:3). Bwana alionyesha kuwa kulikuwa na watu wengi wangojwa wakati wa Yesu lakini ni wale tu waliomjia kwa uponyaji walipata kupona.

Kanuni ya nguvu ya tatu.

IMANI KATIKA MUNGU HUMFANYA MUNGU KUKUTANA NA MAHITAJI YETU.

Imani ni kuamini na kutii Mungu katika kitendo sio tu kwa maneno matupu.(1 Wakorintho 2:2-5). Imani inahusu matakwa na matarajio kulingana na neno la Mungu na ahadi(na yeye ni nani). (Hesabu 23:19). Ili Roho Mtakatifu aweze kujidhihirisha watu hawana budi kuungana zaidi kuliko tu kwa maneno, nyimbo na maombi.(Mathayo 15:8-9). Imani matakwa na matarajio kwa Bwana kufanya kile anachokisema lazima iwepo. Imani huhusisha ,shukrani,sifa na kutangaza matendo makuu ya Mungu(ya zamani, ya leo na siku zijazo) ahadi, tabia au sifa(upendo, hekima, nguvu n.k). utiifu kwa mwongozo na kuelekezwa na Roho Mtakatifu ni muhimu sana ili kumruhusu Roho Mtakatifu kufanya lile analolitaka. Wakati imani na matendo huungana, uwepo wa mungu na nguvu hudhihirika.

Mwanamume mmoja aliletwa katika mahudhurio yetu kanisani akiwa ametoka makao ya kumnasua na kumuuguza(Rehabilitation Nursing Home). Alikuwa amehusika katika ajali ambapo alirushwa futi hamsini kutoka kwenye gari lake na kuvunjika mifupa kumi na mitatu. Ilikuwa muujiza kuwa alikuwa hai. Alikuwa akitarajia kupokea kutoka kwa Mungu. Katika maombi Bwana alimguza na uchungu wake wote ukaondoka wakati huo huo. Mifupa kumi na mitatu iliyokuwa imevunjika iliponywa. Aliweza kugusa vidole vyake vya miguu kwa mara ya kwanza maishani , kisha akajazwa Roho Mtakatifu na akaanza kunena kwa lugha mpya akimpa Mungu shukrani.

Mwanamume mwingine alikuwa akitazama kipindi chetu kwenye runinga”Upendo Wa Mungu” na Mungu akawasha tumaini na imani ndani yake. Alihusika katika ajali akicheza kandanda(Mpira wa miguu). Mguu wake uliteguka vibaya sana na hangeweza kutembea vizuri. Mguu mmoja uliangalia upande. Baada ya kupasuliwa mara nyingi aliambiwa kuwa hakuna lolote lingine lingeweza kufanyiwa mguu wake. Alikuwa kanisani akitarajia muujiza kutoka kwa Mungu. Alipoulizwa sababu yake ya kuja , alijibu,”Nilikuja kuponywa”. Nguvu za Mungu ziligusa mwili wake na akaanguka sakafuni. Miguu yake ilitingika na ikarudi vizuri pahala pake na kuwa sawa kama desturi. Alisimama na kuaanza kukimbia akizunguka ukumbi, akimshukuru na kumsifu mungu.

Naye mwanamke aliyekuwa amechunguzwa na kupatikana na neva za macho zilizokufa akiwa kipofu kabisa kwa miaka mitano alikuwa kanisani kuomba kwa sababu rafikiye aliweza kutoa kitata kilichofungwa mgongo wake kwa sababu Mungu alimponya. Katika mstari wa maombi nguvu za Mungu zilimjia huyu mwanamke na akaanguka sakafuni . Aliposimama alisema ,”Kuna kitu kibaya au kiovu ambacho kimeniondoka mwilini! Alipotazama, alianza kuona mwanagaza, maumbo mitindo, rangi, vitu na watu. Alifurahi pamoja na kila aliyemwona wakati wa utambuzi wake . Alipoulizwa kilicholeta hali hii ya upofu, alieleza kuwa kabla ya hali hii ya upofu kutoke, alikuwa amehusika katika kesi iliyokuwa na uchungu ulioandamana na dhiki. Kesi hii ilikuwa kati yake na rafiki yake. Asubuhi moja aliamka akiwa kipofu na akiwa amepoteza kila kitu chake. Ile siku ambayo alipokea uponyaji wake , tulikuwa tukifundisha kuhusu mianzo mipya. Bwana akadhibithisha neno lake kwa ishara na matendo ya ajabu kufuata. Huyu mwanamke alisema, “Mungu amenipatia mwanzo mpya”.

Katika Matendo ya Mitume 3, Petro na Yohana waliulizwa kuhusu kupona kwa kiwete aliyekuwa akiomba sadaka mlangoni mwa hekalu. Jawabu lao lilikuwa,”*Ni kwa imani katika jina la Yesu, jina lake limemtia nguvu mtu huyu mnayemwona na kumjua; na imani ile iliyo kwake yeye imempatia huyu uzima huu mkamilifu mbele yenu nyinyi nyote*”

Kanuni ya nguvu ya Nne

UWEPO WA ROHO MTAKATIFU LAZIMA UKARIBISHWE, UENZIWE NA UTIIWE.

Ili uwepo wa Mungu na nguvu zake kuwepo, mwanadamu lazima atamani, aenzi au aheshimu na aruhusu Roho Mtakatifu awepo na kufanya lolote Mungu atakalo. Tunapomhudumia Roho Mtakatifu na kupitia kwa Roho Mtakatifu, yeye atatuhudumia.

Tunachokianguzia katika huu wakati wetu, vipawa na mali yahitaji kutoa heshima na kunyenyekea kwa Roho Mtakatifu (Kudhihirishwa kwa Roho wa Mungu kutamjia mtu kama yule na mahali kama pale jinsi Bwana atakavyamua wakati na jambo atakalolifanya.) Lazima tumngojee Bwana na kufanya lile atakalotwelekeza kwalo.

Watu wanaoanguzia mahitaji yao wenyewe au wale wanaojua kuwa wana dhambi ambazo hawajazitubu katika maisha yao humhuzunisha Roho Mtakatifu. (Waefeso 4:17-6:9). tunapomwabudu Bwana kupitia maisha ya utiifu (kama mahekalu yake, Roho wa Bwana anaheshimiwa. (Wakorintho 6:9-20, Warumi 12:1-2 na Wakorosai 3) Fungua moyo na fikra zako kwa Mungu na atajidhihirisha yeye mwenyewe kwako.

Tunapochangua kutomtii Bwana katika maisha yetu Bwana naye hawezi kutembea katika maisha yetu. Watu ambao ni waasi, wenye tamaa, wajitengemeo, wabinafsi na wasiotii hawatauona mwondoko Mungu mpaka wanyenyekee na wamombe Mungu msamaha. Tayarisha moyo wako na fikra kuwa katika uwepo wa Mungu. Kuwa na njaa na kiu ya Mungu kufanya alitakalo. Matokeo yatakuwa mwondoko wa Mungu katika haki, amani na furaha katika Roho Mtakatifu. (Warumi 14:17).

Inatulazimu tuwe na masikio yasikiayo na ulimi uliofundishwa. (Isaiya 50:4-5). Yesu hakufanya au kusema lolote ambalo Babake hakumapatia aseme au afanye. Alimtii Roho Mtakatifu alipowahudumia watu. Jambo hili liliruhusu mapenzi ya Mungu na uwepo wake kuwabariki watu wale. Pia alikutana na mahitaji yao katika nguvu.

Leo kama ilivyokuwa Thesalonike, watu mara nyingi huzimisha moto wa Roho Mtakatifu kwa kutokaribisha ama kutoruhusu udhihirisho wa Mungu katika maisha yao au kanisa. (1 Wathesalonike 5:16-24) ni kama kwamba watu hupitia tu vipindi vya kumwabudu Mungu hawamwamini au hawamuruhusu Bwana adhibitisha kuabudu kwao, maneno na matendo yao kwa uwepo na nguvu zake, angalia jinsi Bwana alivyoendelea kudhihirisha uwepo wake katika Biblia. (Hesabu 17, Kutoka 34, 40, 2 mabo ya nyakati 5-7, 1 Wafalme 8, 18:16-46, 2 Mamba ya Nyakati 20, Matendo ya Mitume 16:25-40, Matendo ya Mitume 2, 4 na 5, Mariko 16:15-20) Mungu wakati kuonyesha uwepo wake na nguvu zake. Watu huimba nyimbo kadhaa, husikiza maandiko au chochote, wanaweza kuomba na watoke baada ya saa moja kwa sababu wana mengi ya kufanya, watu wa kutembelea na mahali pa kwenda. Hii ni heshima kwa Mungu? Ikiwa Mungu alifikiria hivi angedhihirisha uwepo wake na nguvu.

Hawampatii Mungu wakati atembee kwa sababu jambo hiliki litapangua ratiba zao. Lakini ukweli ni kuwa hawatarajii Mungu kutenda lolote kwa sababu yeye hajapangiwa au kutarajiwa kufanya lolote. Mekanisa mengi hayatoi mwito kutoka madhabahuni, hayatoi mwito wa uponyaji au wakati wa Mungu kufanya anayofanya katika Biblia.

Nawambia watu, "Tuko hapa kumuenzi Yesu, tutakuwa hapa mpaka Mungu amalize lile alilotaka kulifanya," (Dakika mbili, masaa mawili, siku mbili, wiki mbili n.k.)

Ikiwa unataka kuona dhahirisho la uwepo na nguvu za Mungu huna budi kukubali na kutii kumngojea kisha umruhusu kufanya alitakalo. Lazima umakinike na uadabike kama Danieli aliyengoja, akifunga na kuomba kwa kila siku ishirini na moja mpaka akalipokea jibu.(Danieli 10)

Je , na mtu akianguka na afe kanisani? Tutatamatisha hudhurio au tutafanya vile Paulo alifanya: kumfufua kutoka wafu katika jina la Yesu na kuendelea na mahubiri? (Matendo ya Mitume 20:7-13) na ufanyiwe kulingana na imani yako. Je, mungu anaheshimiwa na kukaribishwa au la? Je yumo au la?.

Kuongea katika Roho (lugha) kunatia imani yako nguvu kulingana na neno la Mungu. (Wakorintho 14:14-15, Yuda 20). Si ajabu kuwa imani ya watu haitiwi nguvu, makanisa mengi hayaamini katika kunena kwa lugha ama huzuia matumizi yake.. jambo hili huzima moto wa Roho Mtakatifu. Neno la Mungu lasema , “Takeni sana kuhutubu wala msizuie kunena kwa lugha. Lakini mabo yote na yatendeke kwa uzuri na kwa utaratibu.

Mwanadamu hutaka sana kutawala kuliko kumwachia Mungu atawale maisha na kuabudu. Mpangilio wa Mungu sio wa mwanadamu ndio sheria. (Wakorintho 14 hutoa mpangilio ufaao) Nani hutoa ule mpangilio? Ingekuwa afadhali ni watu wanaomwamini Bwana na wanaoruhusu kudhahirishwa kwa Roho wa Mungu. (1 Wakorintho 12-14, Warumi 8:5-15) hao ndio waliohitimishwa na Mungu kujaribu Roho na kujua yaliyo ya Mungu na yasio yake. Kutoamini na kutotii huzima moto wa Mungu hivyo kumfanya mtu asihitimu kuzijaribu roho.

Ishara za Roho Mtakatifu haziwezi kujaribiwa kwa akili au hisia za mwanadamu ila kwa roho wa mwanadamu(akiwezesha na Roho Mtakatifu) na tunda (matokeo) kazi ya Roho Mtakatifu italeta matokeo ya haki, amani na furaha (Warumi 14:17). baadhi ya matokeo ya uwepo na nguvu za Roho Mtakatifu ni:

- 1.Kutubu.
- 2.Uponyaji wa kifikra, kimwili au kimahusiano.
- 3.Kukombolewa kutoka nyanyaso za kishetani.
- 4.Wokovu.
- 5.Kujazwa Roho Mtakatifu.
- 6.Kudhahirisha na kukataa majaribu.
- 7.Mabadiliko katika maisha.
- 8.Watu kumkaribia Mungu sana ambapo upendo mkubwa na kumtegemea kutatokea. Kuwapenda wengi kutaongezeka. Ikiwa neno la Mungu ni kweli kuwa mbele za uso wako ziko furaha tele (Zaburi 16:11), kwa nini wakristo wengi huwa na huzuni tele ndani na nje ya kanisa? Pengine hawamo katika uwepo wa Mungu. Uwepo wa Mungu na nguvu huwafanya watu kuwa na furaha. Uwepo wa Bwana huleta upendo wa Mungu, nguvu, hekima, amani na furaha, ukiharibu kazi za mwovu shetani na kujenga ufalme wa Mungu. Yesu alisema, “*Kwa kuwa walipo wawili watatu. Wamekusanyika kwa jina langu, nami nipo hapokatikai yao*” (Mathayo 18:19-20).

Kanuni ya nguvu ya tano

PALIPO WATU WANAOMBA, NGUVU ZA MUNGU HUTAKUJA ZITASHUKA.

Kuomba ni kuwasiliana na Mungu. Hutangulia mwondoko wowote wa Mungu. “*Ikiwa watu wangu, walioitwa kwa jina langu, watajinyenyekesha, na kuomba, na kunitafuta uso, na kuziacha njia zao*

mbaya, basi nitasikia toka mbinguni, na kuwasamehe dhambi zao, na kuiponya nchi yao. (Mambo ya Nyakati 7:14)

Yesu aliwaagiza wanafunzi wake kungoja na kuomba kwa ajili ya kudhihirishwa kwa nguvu za Roho Mtakatifu wakati wa Pentekoste, wakati ambapo wanafunzi wote walijazwa Roho Mtakatifu na kunena kwa lugha. Watu elfu tatu waliokoka siku hiyo ya kwanza ya kanisa, wanafunzi walipopata nguvu kwa Roho Mtakatifu.

Kufuatia dhihirisho hili la nguvu za Mungu, adha au mateso ya kwanza katika kanisa yalitokea. Watu waliomba pamoja ili wawe na ushujaa zaidi wa kuhubiri. Waliomba kuwa katika jina la Yesu hata ishara kubwa na miujiza ya nguvu za Mungu ikatendeka kuthibitisha neno lake. Waliendelea kuomba bila kusita na kutamani dhihirisho kubwa la ishara za Mungu, miujiza na uponyaji miongoni mwao ili kumtukua Mungu. Matokeo yalikuwa kutingisika kwa kuta za mahali walipokuwa wamekutana. (Matendo ya Mitume 4:27-37) katika Matendo ya Mitume 5 ishara na nguvu ziliongezeka.

Yesu mara nyingi alikuwa akitoka na kuenda mahali pasipokuwa watu kuomba. (Luka 4:42, 6:12) ni nyakati kama hizi alikuwa akipokea mwelekeo na maagizo kutoka kwa baba yake wa mbinguni kuhusu kile angekitenda na vile kingetendeka. Matokeo ya wakati wa kujitenga na kuwa peke yake na Mungu jinsi hii yalionekana katika nguvu za Mungu zikitenda mapenzi yake. Utiifu wa Yesu katika mwongozo wa babake ulidhihirisha nguvu zake.

“Niite, nami nitakuitika, nami nitakuonyesha mambo makubwa, magumu usiyoyajua” (Yeremia 33:3)

Kote katika neno la Mungu kuna mifano ya kudhihirishwa kwa nguvu zake kulikotokea wakati watu wake, akiwa mmoja au wengi pamoja, walimwita Bwana awasaidie au waliamua kumpa nafasi ya kwanza.

Watu wanaoshuhudia matokeo ya nguvu za Mungu huwa wametumia muda wao katika uwepo wake, wakisikiliza na kuzungumza naye.

Maombi si mawasiliano ya njia moja pekee. Tumwombapo Mungu tunapaswa kumsikiliza atupatie jawabu na tufanye vile anavyosema, kuyatenda matendo yake. Tarajia nguvu zake kuachiliwa katika jina la Yesu wakati unapoomba na utashuhudia.

Tenga wakati mzuri wa kuwa na Mungu, msikilize zaidi ya unavyoongea. Badhi ya watu wana kazi nyingi ya kuzunguka wakifanya kazi ya kidini kiasi kwamba hawawezi kusita ili wawe na Mungu na waweze kujua kama anawataka wafanye kile wanachokifanya! Yesu aliomba saa nyingi. Wanafunzi hawangevumilia hata kwa saa moja. Leo watu wengi kanisani hawawezi kuomba hata kwa dakika kumi wanaajabia kwa nini hawapati matokeo ya maombi yao kutoka kwa Mungu. Maisha ya kufunga na kuomba humruhusu mtu amtumainie na kumtegemea Mungu katika mambo yote (Mithali 3:5-6) na huweza kujinyima nafsi zetu. Tamaa kubwa ya mtu hapa ni kujua na kufanya kile Mungu akitakacho (Isaiya 58), matokeo yakiwa utukufu wa Mungu unaodhihirishwa katika nguvu.

Kanuni ya nguvu ya sita.

HURUMA, SIO KUCHUKUANA KATIKA UDHAIFU, HUZAA MIUJIZA

Katika Biblia huruma huongoza nguvu za Mungu. Alipoona moyo wa watu wa kutaka ukweli wa Mungu na njaa yao ya kiroho na kimwili, Yesu aliwahurumia. (Mathayo 14:14,15:24-32, Yohana 6:29) huruma hutoka kwenye moyo wa Mungu wa kupenda na kuwajali watu wake wanaloiti jina lake na kutafuta uso wake (Yona 4:2). Bwana huonyesha rehema zake kwa yule amtakaye.

Huruma, sio kuchukuana katika udhaifu. Kuchukuana katika udhaifu hudumisha watu katika hali zao. Yesu huchukuana nasi katika mambo yetu ya udhaifu kwa kuwa alipitia yale tuyapitiayo. Anajua mahitaji yetu. (Waebrania 4:14-16) hata hivyo maisha yake, kifo na kufuka kwake zilikuwa ni tendo la huruma ya Mungu kutuwezesha kukaribia kiti cha neema kwa ujasiri, (imani) ili tupewe rehema (Uwezo) na neema ya kutusaidia wakati wa mahitaji.

Kuchukuana katika udhaifu huelewa na hujitambulisha na maumivu na uchungu (pathos) huruma humfanya mtu kumwamini Mungu na kuibadilisha hali yake kwa neema na nguvu za Mungu. Huruma ni hali ya Mungu ya upendo kuingilia kati hali zetu, ikiwezesha imani katika Mungu wala si matatizo kuyatawala maisha ya mtu (Luka 7:13-17).

Watu hawahitaji hali hii ya kuchukuana katika udhaifu wakati wanapopitia matatizo mbalimbali. Maskini wee! Wanahitaji kusikia, “Mungu ni mkuu kuliko yale unayoyapitia. Amini Mungu na atakufanya mshindi. Hiyo ndiyo huruma. Huruma hutokana na Mungu na huzaa unyenyekevu (Kumtegemea Mungu) na ukweli.

Kuchukuana katika udhaifu hudumisha watu katika matatizo yao kwa kujitambulisha na kujizoesha tatizo. Watu wanaotaka hali hii ya kuchukuana katika udhaifu hawataki suluhisho au msaada. Kiburi huwadumisha katika matatizo yao kwa sababu hawataki kumwamini Mungu awasasi huhurumiana.

Kinyume na hali hii ya kuchukuana katika udhaifu, huruma ya Mungu huwatoa watu katika matatizo yao kwa kuangazia Mungu kusuluhisha matatizo yao. Huruma humwingiza mtu ndani ya imani katika Mungu na kuachilia nguvu za Mungu kuufanya miujiza.

Huruma inapodhihirishwa, hubadilisha kiangazio cha mtu kutoka “Maskini mimi” hadi “Bariki Mungu”. Wakati huu mtu haliangalii tatizo lake bali huangalia suluhisho kutoka Mungu au riporti ya sifa kwa yatakayotendeka. Huruma ya Mungu huongoza, hutarajia huamrisha nguvu zake kuinuka na kufanya kazi. Upendo wa Mungu hudumu milele. Imani ya Mungu hutenda kwa upendo wake na huleta nguvu zake na matokeo.

Kanuni ya nguvu ya saba

WATU HAWANA BUDI KUTAKA MABADILIKO YA KIMAISHA AU HALI.

Ili kutayarisha mazingira mwafaka ya nguvu za Roho Mtakatifu, watu hawana budi kutaka alichonacho Mungu kwao. Lazima watake uhai tele ulioahidiwa na yesu na lazima wamtegemee na kumwamini gu kuwa atatenda jambo hili.

Katika vitabu vya injili, Yesu hakuponya yeyote aliyekuwa mgonjwa. Aliponya wale tu waliokuja kwake kuponywa. Aliponya yeyote aliyekuja kwake. (Mathayo 8:16-17, 9:35-36, Luka 6:17-19) nguvu za Mungu ziliwafikia wale waliotaka na waliohitaji mabadiliko katika maisha yao na hali

zao.

Watu kuwa wagonjwa hakumaanishi kuwa wanataka kupona. Sababu watu hawajaokoka haimaanishi kuwa wanataka kuokoka. Kwa vile watu wamefungwa haimaanishi kuwa wanataka kukombolewa. Hata hivyo wangetaka haya yote lakini hawana imani ya kupokea. (Mariko 9:20-24).

Ili nguvu za Mungu kudhihirika, watu lazima wanyenyekee na kumtafuta Mungu vilivyo kwa mioyo yao yote, wakitambua mahitaji yao na kumwamini kukutana nayo.

Kama ilivyosemwa awali mfalme Asa alitaka kumtafuta Mungu na kuwategemea waganga pekee, alikufa kwa sababu ya ugonjwa wa mguu kwa vile hakuna nguvu zilizotoka kwa Mungu.

Mwanamke aliyetokwa na damu (Luka 8:42-48, mariko 5:24-34) alikuwa mgonjwa kwa miaka kumi na miwili. Alikuwa amegharimiwa mali zake kwa kuwapa waganga na hakupata kuponywa na yeyote. Aliwaza, "Ikiwa tu nitaguza vaiz lake nitapona" Yesu alijua kuwa ule wakati mwanamke alinguza nguvu zilimtoka.

Yesu alimjibu akamwambia, "*Binti imani yako imekuponya, enenda zako na imani*". Imani yake iliachilia nguvu za Mungu kupitia kwa Yesu. Alitaka mabadiliko kwa hivyo aliyatafuta na kumwamini Mungu kuyatekeleza. Nguvu za Mungu zilifanya hivyo.

Katika mwaka 1975 wakati Mungu alikuwa akinifunza kuhusu nguvu zake, mtu mmoja aliongea nami kuhusu mke wake aliyeugua ugonjwa wa saratani. Alikuwa amesikia kuhusu miujiza nguvu za Mungu zilikuwa zinatenda. Tulienda kuomba na mke wake. Nilihisi nguvu za Mungu zikinitoka na kumfikia na tena kunirudia. Nikamwomba atoke kitandani na kunawa uso wake kama tendo la imani. Alinijibu, "Siwezi kufanya hivyo. Mimi ni mgonjwa sana" Tulienda katika chumba kingine. Mumewe akampokea Yesu moyoni mwake kama Bwana na mwokozi na akajazwa Roho Mtakatifu na pia kunena katika lugha mpya.

Baada ya siku kadhaa nilisoma kwa gazeti kuwa ameaga dunia. Pia nami niliugua na nikaanza kuzishuku nguvu za Mungu na pia imani yangu. Sauti ilinijia mawazoni mwangu, "Tabibu umewaponya wengi, kwa nini usijiponye mwenyewe?"

Kufishwa moyo na shetani kulinizindua na imani ya Mungu iliinuka ndani yangu. "Katika jina la Yesu, ondoka katika mawazo yangu na mwili wangu! Kwa mapigo ya Yesu nimepona." Neno la Mungu ni kweli kama naliona au kuhisi.

Bwana aliendelea kuniongoza katika mawazo yangu nirudi kwa yule mtu ambaye mke wake alikufa Mungu aliniambia "Kusanya ukweli wote." Yule mtu alinikaribisha na kunieleza kile kilifanyika siku baada ya kutembea kwake. Mke wake alikusanya pamoja familia yote, akawatayarisha kuhusu kifo chake (kilichotokea siku iliyofuata). Hakuamini kuwa angeishi bali kufa. Nilikuwa na ithibati kuhusu alichokiamini mama huyu. Imani yetu na maombi yalikuwa mazuri hakuwa amepokea nguvu za Mungu za kuponya kwa sababu aliamini kuwa angekufa.

Bwana alinihimiza kukusanya ithibati zote kuhusu yale wanayoamini watu. Itatendeka kulingana na imani ya watu. Nilielewa kile Yesu alikuwa akimwambia yule mtu aliyemjia kuhusu mtoto wake. (Mariko 9:17-19). yule mtu alimwambia Yesu, "Ukiweza nena lolote, utuhurumie na kutusaidia" Yesu akawaambia, ukiweza yote yawezekana kwake aminiye."

Halikuwa swala la nguvu za Mungu kuwepo ili kuponya bali kuwepo kwa imani ili kuachilia nguvu za Mungu. Yule mtu alimjibu”Naamini nisaidie, kutoamini kwangu.” Nguvu za Mungu zilimweka huru yule kijana wakati Yesu alipomwamuru yule pepo atoke. (Tazama Luka 10:19-20)

Baadhi ya watu hawaamini katika urejesho katika ndoa, uponyaji au ukombozi, wengine hawataki kupoteza faida za bima. Ikiwa hutaki ndoa yako idumu au unataka kuishi nje barabarani, usitarajie nguvu za Mungu kuenda kinyume na mapenzi yako na chaguo lako. Huwezi kusema kuwa nguvu za Mungu hazifanyi kazi wakati ambapo hutaki mabadiliko.

Mwanamke aliyekuwa mgonjwa mahututi angeponywa na nguvu za Mungu kila wakati tulipomwomba. Hata hivyo baada ya wiki moja au mbili angeugua tena.

Nilipoanza kumwomba, Bwana alizungumzia mawazo yangu, “Usimwombe! Anataka kuwa mgonjwa” Nikawaza, nani angetaka kuwa mgonjwa? Kweli yeye alitaka. Akiwa mgonjwa, mumewe alitakiwa kukaa nyumbani ili amsaidie. Alitaka kujaliwa..... na kutawala. Mumewe alikufa kabla ya mwanamke huyu. Je ungetaka na kuruhusu nguvu za Mungu kubadilisha na kubariki maisha yako?

Kanuni ya nguvu ya Nane

NENO LA MUNGU NA UKWELI ZIPO KUACHILIA NGUVU ZAKE

Angalia mifano hii kutoka kwa neno la Mungu.

1. Bwana anayataja yale yasiyokuwa kana kwamba yamekuwako.

(Warumi 4:17)

2. Bwana akasema, “Na iwe.....” na maumbile yakatokea.

(Mwanzo 1)

3. Bwana hilituma neno lake, huwaponya.

(Zaburi 107:20)

4. Bwana hulidhibitisha neno lake kwa ishara zinazofuatana nalo.

(Mariko 16:19-20, Matendo ya Mitume 14:3)

5. Wale wataoendelea kukaa katika neno la Mungu, ndio wanafunzi wake kweli kweli, tena wataifahamu kweli nayo hiyo kweli itawaweka huru (Yohana 8:31-32)

6. Mungu atatenda analolisema. (Hesabu 23:19)

7. Neno lake ni Roho na uzima (Yohana 6:63) nguvu za Mungu zitaonekana mahali ambapo watu wanamuuliza Roho Mtakatifu awalettee neno la Mungu. Hatuna budi kumuuliza Roho Mtakatifu atupatie kile Mungu wala si mwanadamu anataka kusema. Mahubiri mengi na hata yale yaliyotolewa kwa Biblia sio neno la Mungu kwa watu wake Bwana alionyesha kuwa unaweza kuongea kutokana na neno katika Biblia lakini si neno la Mungu kwa sababu halijachochewa, halijaongozwa na kuamrisha na Roho Mtakatifu. Bwana atadhihirisha nguvu zake wakati neno lake la wakati ule limenenwa chini ya mwongozo wa Roho Mtakatifu.

Kanuni ya nguvu ya Tisa

NENO LA MUNGU KUPITIA KWA MANABII WAKE LAZIMA LIHESHIMIWE.

Mazingira ambayo Mungu atadhihirisha nguvu zake ni yale ambayo neno lake litanenwa na

watumishi wake. Neno la Mungu lina nguvu na ni kweli, hata hivyo lazima liaminiwe, liheshimiwe, lienziwe na kutiwa na watu ili liwe na nguvu katika maisha yao. Neno Mungu pamoja na watumishi wake lazima liheshimiwe ili nguvu zake kuonekana.

Neno linasema, *“Mwaminini Bwana Mungu wenu, ndivyo mtakavyohibitika, waminini manabii wake, ndivyo mtakavyofanikiwa”* (2 Mambo ya Nyakati 20:20, Hesabu 33:8, Matendo ya Mitume 28:10) Paulo anamshukuru Mungu kila wakati kuwa watu walipokea na kulikubali neno la Mungu kupitia kwake. Walisikia neno na sio kama maneno ya mwanadamu wa kawaida lakini kama neno lilivyo- neno la Mungu. Neno hili linafanya kazi kwa wale wanaliamini (1 wathesalonike 2:13, 4:8, 5:12-13)

Shetani anataka kudhalilisha ujumbe wa Mungu na wajumbe wake. Anaaminisha watu wasiwaamini au kuwafanya waamini kwamba wajube hawa si wa mungu. (Mathayo 12, 10:24-25) Bwana ametenga, kupaka, kuwapa nguvu na mamlaka watumishi wake katika mwili wa Kristo kwa kusudi la kuwakamilisha hata kazi ya huduma itendeke, kutenda mema na kuharibu kazi ya shetani (Wafeso 4:11-16, Matendo ya Mitume 10:38)

Watu lazima wawaamini na kuwaheshimu watumishi wa Mungu ikiwa wanataka kuona nguvu za Mungu katika maisha yao. Huko Nazareti, Yesu hakudhihirisha nguvu za Mungu kwa sababu watu hawakumwamini Mungu, hawakumwamini Yesu au kuamini kuwa Mungu alitenda kupitia kwake. (Mariko 6:1-6)

Ukitafuta neno la mchawi utabarikiwa na shetani na ni chukizo kwa Bwana Mungu. (Kumbukumbu la Torati 18) ukilitafuta neno la Bwana kupitia watumishi wake utaziona nguvu za Mungu zikifunuliwa, kwa kuwaheshimu na kuwaamini watumishi wa Mungu, unamheshimu na kuleta yaliyo mazuri kutoka kwake kupitia watumishi wake hadi kwako, (1 Wathesalonike 5:12-13)

Kanuni ya nguvu ya kumi

UMOJA HULETA NGUVU ZA MUNGU

Watu wanapokusanyika pamoja wakiwa na moyo mmoja, mawazo na kusudimoja, mazingira yanayoruhusu nguvu za Mungu kudhihirika hutokea. Kwa upande mwingine, utengano huzuia Roho wa Mungu kutembea.

Yesu alisema, *“Kwa kuwa walipo wawili watatu wamekusanyika kwa jina langu, nami nami nipo hapo katikati yao”* (Mathayo 18:20) *“Wawili wenu watakapokutana duniani katika jambo lolote watakaloliomba, watafanyiwa na Baba yangu aliye mbinguni”* (Mathayo 18:19)

Wakati watu wanapokusanyika pamoja kataika Yesu, wakitamani tu kumheshimu na kumwabudu, Bwana atawakaribia. Jisahau wewe mwenyewe na mahitaji yako, hisia zako au mawazo. Tamani kumpenda Yesu na watu. Amini Mungu kugusa kila mtu kwa njia ya kipekee jinsi Bwana atakavyo. Tarajia Bwana atende analolitaka. Kwa furaha na shukrani karibia Bwana pamoja na ndugu zako katika Kristo kutoka mataifa yote. Sisi sote ni sawa katika Yesu. Hushirikiana katika huzuni, tukitarajia Mungu kuyageuza machozi yetu kuwa ripoti ya sifa zenye furaha. Tunamwamini Mungu pamoja kwa ushindi. Mungu atakuwepo katika hekima na nguvu.

Wakati tunapokana nafsi zetu na kumfuata Kristo Yesu, tunakusanyika pamoja na Mungu na wengine waliokwisha fanya hivyo. Neno la msalaba ndilo nguvu ya Mungu kwa wale wanaookolewa. (1 Wakorintho 1:18) Neno la msalaba pia ndilo neno la umoja katika Kristo Yesu ambaye ndiye hekima na nguvu za Mungu (1 Wakorintho 1:23-24) Yesu anapohubiriwa, hekima na nguvu za Mungu zitadhihirika. Yesu anapoinuliwa, atawaleta watu kwake. Wote waliokataa nafsi yao na kumpokea Yesu kama Bwana wao huwa sawa ndani yake (Yohana 17) umoja huu katika upendo ni dhihirisho la nguvu za Mungu wetu katika ulimwengu katika jina la Yesu.

Muhutatasi wa mazingira ya Roho Mtakatifu.

1. Jua na uamini kuwa Bwana ni mwenye upendo, huwepo, mwenye huruma na mwenye nguvu.
2. Watu wana mahitaji ya kutimiziwa.
3. Imani katika Mungu humfanya Mungu kukutana na mahitaji yetu.
4. Uwepo wa Roho Mtakatifu lazima ukaribishwe, uenziwe na utiiwe.
5. Palipo watu wanaoomba nguvu za Mungu zitashuka.
6. Huruma sio kuchukuana katika udhaifu, huzaa miujiza.
7. Watu hawana budi kutaka mabadiliko ya kimaisha au hali.
8. Neno la Mungu na ukweli zipo kuachilia nguvu zake.
9. Neno la Mungu kupitia manabii wake lazima liheshimiwe.
10. Umoja huleta nguvu za Mungu.

© 1997, Dr. Randy Brodhagen, Glory To God Ministries International™,
all rights reserved,

www.glorytogod.org